



TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega (Nzega WSSA) (“Muombaji”) kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Mji Mdogo wa Nzega, Mkoa wa Tabora. EWURA inakaribisha maoni kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Muombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:

1: Jina na Anuani:

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega,
S.L.P 145,
Nzega.
Barua Pepe: mdnzega@maji.go.tz

2: Maelezo ya Leseni:

Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji mdogo wa Nzega

3: Vyanzo vya Maji na Miundombinu

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega inatoa maji kutoka vyanzo vitatu (3) ambavyo ni bwawa la Uchama, Visima na maji ya jumla kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA). Jumla ya uwezo wa kuzalisha maji kwa maeneo yote ni mita za ujazo 12,880 kwa siku ambazo zinatoshleza mahitaji ya maji ya wastani wa mita za ujazo 5,664 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji ina uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 4,450. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 465 pamoja na vilula mia moja na kumi na nne (114).

4: Umiliki

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi
S. L. P 2857, Dodoma.

Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;

Namba ya Bure 0800110030;

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu

EWURA